HOTUBA YA MKUU WA SHULE BIBI HALIMA KAMOTE KWENYE SHEREHE ZA MAADHIMISHO YA MIAKA 19 YA SHULE NA MAHAFALI YA 17 YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA NNE YA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA BARBRO JOHANSSON; JUMAMOSI TAREHE 28 SEPTEMBA 2019, LUGURUNI, DAR ES SALAAM

Mgeni wetu Rasmi, Mheshimiwa Bi Gladness Deogratias, Mkuu wa Kitengo cha Masoko ya fedha, Idara ya Hazina,

Mh. Anders Sjoberg, Balozi wa Sweden nchini Tanzania;

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Shule Bwana Raymond Mapunda, na Wajumbe wa Bodi ya shule,Waanzilishi na wajumbe wa Bodi ya Wadhamini;

Mhe. Dweza H. Kolimba Diwani wa kata ya Kwembe na viongozi wengine wa kata na mtaa wa Kwembe;

Mwakilishi wa Afisa Elimu Sekondari, Bibi Shima Banele, Afisa Elimu Vifaa na Takwimu, Manispaa ya Ubungo;

Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi na Walimu (PTA), Dr. John Kyaruzi na Kamati nzima ya PTA ya sasa na zilizotangulia;

Wakuu wa Shule, Walimu na Wanafunzi kutoka Shule za Sekondari na Msingi ambazo ni jirani na jirani na rafiki;

Bibi Katarina Heide, Makamu Mkuu wa Shule, Mwalimu Nina Ejlertsson na wanafunzi kutoka Procivitas Privata Gymnasium, Sweden

Wahitimu wa Kidato cha 4 na wanajumuia wa Shule ya Barbro Johansson;

Viongozi wa Dini;

Wazazi na Wageni waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Itifaki imezingatiwa,

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,
Ni furaha na heshima kubwa kwangu kuwakaribisha nyote, viongozi wetu wa serikali, marafiki kutoka Sweden, wakuu wa Shule za Sekondari na Walimu wakuu wa Shule za msingi, wazazi na wana familia, walimu, wanafunzi na zaidi sana wahitimu wetu wa kidato cha nne.

Kwa namna ya pekee naomba nitoe shukrani zetu za dhati kwako wewe Bi Gladness kwa kutenga muda, katika ratiba yako ngumu, kushiriki pamoja nasi katika sherehe hizi za kuadhimisha miaka 19 ya Shule na mahafali ya 17 ya kidato cha nne. Naamini ujio wako hapa kwetu utatia hamasa katika mioyo ya wasichana wetu ili nao wajitolee katika kuhudumia jamii.

Nakushukuru wewe Mheshimiwa Balozi Anders Sjoberg kwa kutenga muda ili uwe pamoja nasi siku ya leo, bila kusahau rafiki zetu wa Procivitas Privata Gymnasium kutoka Sweden ambao wameweza kushiriki katika hafla hii. Natumia pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wale wote walioandaa shughuli hii hususan wafanyakazi na wanafunzi wa Shule ya Barbro. Namshukuru kila mmoja wenu kwa ushiriki wake.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana;
Haitakuwa rahisi kusema yale yote yaliyotokea kwa miaka 19 iliyopita, kutokana na muda kuwa finyu katika ratiba yetu. Hivyo nitajikita katika kuelezea historia kwa ufupi, baadhi ya mafanikio, kuwatambua washirika wetu katika maendeleo, kuelezea changamoto na hatimaye kutoa neno la busara kwa wahitimu.

Kila mwaka sherehe kama hizi hufanyika tarehe 25 Septemba, siku aliyozaliwa Dk. Mama Barbro Johansson, ili kumuenzi mama huyu mmisionari, mwalimu mahiri, mwana harakati na mwana diplomasia. Mama Barbro atakumbukwa daima kwa mchango wake mkubwa katika kupigania elimu si tu kwa mtoto wa kike bali pia kwa mtoto wa kiume. Mwaka jana tuliamua sherehe kama hizi zifanyike Jumamosi inayoangukia wiki aliyozaliwa mama Barbro kwa kuwa ni mwisho wa wiki ili kuwapa fursa wazazi wengi kuhudhuria mahafali kwa uhuru bila kuathiri utendaji wao siku za kazi na ndiyo maana sherehe hii imefanyika leo 28 Septemba 2019, ingawa siku ya kuzaliwa Mama Barbro ilikuwa siku tatu zilizopita.

Mabibi na Mabwana,
Kihitoria Shule ya Barbro ilianzishwa mwaka 2000 pale Ada estate, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, ikiwa na darasa anzilishi la kidato cha I lililokuwa na

wasichana wahitaji 40 kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania; wote kwa wakati huo wakisoma kwa ufadhili wa 100%.

Mwaka 2001, JOHA TRUST Tanzania na mfadhili mkuu kwa wakati huo SIDA kupitia ubalozi wa Sweden, Dar es Salaam, walifikia uamuzi wa pamoja wa kudahili pia wanafunzi ambao wazazi wao wanaweza kulipa ada. Uamuzi huu ulikuwa muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Shule hasa baada ya kukoma kwa ufadhili kutoka kwa wahisani.

Mwaka 2002 Shule ilihamia hapa Luguruni baada ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza katika eneo hili lenye ukubwa wa ekari 50 ambalo tulipewa na Serikali. Hatimaye Shule ilipata msaada mkubwa kutoka Serikali ya Sweden ambao uliwezesha kuweka majengo na miundombinu mingine.

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Katika miaka 19, Shule ya Barbro imekua, kwa sasa tunao wanafunzi 530, kuanzia kidato cha I hadi cha 6. Tunao wafanyakazi 59 wakiwemo walimu 31 na wafanyakazi wengine 28. Masomo yanayofundishwa kwa kidato cha I hadi 4 ni 16 na Tahasusi zipo 10 kwa kidato cha tano na sita katika sayansi, biashara na sanaa, hivyo kuwapa wanafunzi wigo mpana wa uchaguzi wa masomo na tahsusi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Kuna msemo usemao “Mgaagaa na upwa hali wali mkavu”. Shule yetu imepata mafanikio makubwa kimaendeleo tangu ianzishwe miaka 19 iliyopita. Nitayataja baadhi:

Hadi sasa shule imetoa wahitimu 1231 wa kidato cha nne na 1203 wa kidato cha sita. Ukiongeaza na hawa wahitimu 87 wa darasa la kidato cha nne tunapata jumla ya wahitimu wote kutoka shule hii kuwa 2,521. Kati ya wahitimu waliotangulia, 99.9 walifaulu mitihani yao ya taifa katika viwango vya kuwawezesha kuendelea katika ngazi nyingine za elimu. Hivi karibuni matokeo ya Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Sita mwaka huu 2019 yalikuwa ya kutia moyo sana kwani kati ya wanafunzi 146 waliofanya mitihani hiyo , wanafunzi 47 walipata daraja la kwanza, 77 walipata daraja la pili, 22 daraja la tatu, na hapakuwa na daraja la nne wala zero. Kati yao wanafunzi 37 Sawa na asilimia 26 walipanda madaraja ya ufaulu ukilinganisha na ufaulu waliopatakwenye mitihani ya taifa ya kidato cha nne. Hii inadhihirisha utekelezaji kwa vitendo wa sera yetu ya kumsaidia mwanafunzi wa Barbro kufikia uwezo wake wa juu kitaaluma.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mabibi na mabwana;
Shule ya Barbro haikuachwa nyuma katika mashindano mbalimbali yakiwemo kuandika insha, chemsha bongo na mambo yahusuyo taaluma. Mara nyingi tumeibuka washindi kama ambavyo mmejionea kwenye vyeti mbalimbali vya ushindi ambavyo tumevionesha kwenye ubao wa matangazo nje ya jengo la utawala. Vilevile shule imewezesha kukuza vipaji mbalimbali katika uongozi, Sanaa za ubunifu, maigizo, uimbaji, ngoma, muziki wa kisasa na michezo mbalimbali na kujenga mahusiano mema na shule nyingine kitaifa na kimataifa kama ambavyo mmeshuhudia leo tuna shule rafiki zilizowakilishwa kwenye hafla hii kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;
Shule inaendelea kutekeleza mpango wa kuwafikia wasichana wanaotoka kwenye familia zenye uhitaji. Kwa kupitia mpango huu wasichana wanaotokea kwenye familia hizo wengine mbali mikoani, wamefikiwa na wamenufaika. Kwa sasa 10% ya wanafunzi wetu wananufaika na ufadhili wa ada. Tunawashukuru washirika wetu wa maendeleo JOHA TRUST Foundation ya Sweden chini ya Mwenyekiti Mama Gun Britt Andersson kwa kuendelea kuwezesha mpango huu kifedha.

Mheshimiwa mgeni rasmi,
Mwaka kesho tunatimiza miaka 20 tangu shule hii ianzishwe. Kama nilivyoeleza awali tuna wahitimu zaidi ya 2000 ambao wamepita kwenye mikono yetu hivyo wakati tunaadhimisha miaka 20 ya shule tumepanga pia iwe siku kuu ya kukutana tena wahitimu wetu, yaani alumni reunion day. Leo tuna wawakilishi wa wanafunzi wetu waliohitimu Barbro miaka tofauti na kati yao kuna walimu wa Barbro wawili wa madarasa ya mwaka 2000 na 2001 ambao walihitimu hapa shuleni, wakaendelea na elimu yao ya chuo kikuu na hatimaye kurudi tena Barbro kama walimu. Wawakilishi hawa wanaunda kamati ya maandalizi ya siku ya kukutana tena alumni mwaka kesho tarehe 25 Septemba. Baadaye tutakuomba pia mgeni wetu rasmi utoe tamko la kuzindua rasmi kamati hiyo ya maandalizi ya siku kuu ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;
Tunapoongelea juu ya maendeleo tukumbuke kuwa kuna watu ambao wametoa mchango mkubwa kuleta maendeleo hayo. Mradi huu wa shule usingeweza kuwepo bila ya kuwa na waanzilishi mahiri. Naomba kutumia fursa hii kumshukuru Hayati balozi Wilson Tibaijuka ambaye alikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa JOHA TRUST (Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi),

Mwenyekiti Mwanzilishi, Mheshimiwa Professa Anna Tibaijuka, ambaye ameshindwa kuwepo leo kwani yupo Marekani kuhudhuria mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, lakini ametuma salamu zake nyingi kwetu sote, Wajumbe wa Bodi na washauri chini ya Mwenyekiti Bwana Salmon Odunga na Mlezi wa Bodi Balozi Paul Rupia, ambao wametoa muda wao mwingi, akili na nguvu, ili kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa. Napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru wale wote ambao michango yao ya mawazo hali na mali imetufikisha hapa tulipo.

Kwanza kabisa ni Serikali ya Tanzania ambayo imetupatia ekari 50 za ardhi hii ya hapa shuleni ambayo tunajivunia, miundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, maji na umeme, usajili wa shule, ukaguzi, mitihani ya taifa na ushirikishwaji katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;
Shule hii isingefika hapa ilipo kama si msaada mkubwa uliotolewa na Serikali ya Sweden kupitia Ubalozi wa Sweden hapa Dar es salaam kwa miaka 12 kuanzia 2000 hadi 2012. Msaada huu ulitumika kwa ujenzi na kufadhili wasichana waliotokea kwenye mazingira magumu. Niwahakikishie ndugu zetu wa Sweden kuwa mti mliopanda utaendelea kuzaa matunda yatakayolisha wengi kwa muda mrefu ujao.

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;
Kwa wazazi wa wanafunzi wa Barbro, maneno hayatoshi kuonesha shukrani zetu kwa jinsi ambavyo mmeendelea kutusaidia na kuweka uhusiano mzuri na Shule yetu. Naamini moja ya kitu kinachotofautisha Shule ya Barbro na nyingine ni uhusiano madhubuti na uwekezaji wenu katika kuwajali wasichana wetu hawa na wafanyakazi pia. Asanteni sana kwa kushiriki nasi katika maendeleo ya Shule na malezi ya watoto wenu ambao ni tunu bora mliyo nayo. Asanteni kwa kutuamini katika kuwapatia elimu na kuwalea katika maendeleo ya makuzi yao.

Ki uhalisia siyo rahisi kumshukuru kila aliyejitoa kusaidia maendeleo ya shule hii kwa kuwa orodha ni ndefu lakini itoshe tu kusema asanteni sana wote kwa kutuunga mkono.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mabibi na mabwana;
Kuna usemi usemao “Hakuna barabara isiyo na kona”. Pamoja na maendeleo tuliyofikia, Shule inakabiliwa pia na changamoto:

Mosi Mpango Mkuu wa Shule (Master plan) haujakamilika ikiwemo majengo ya ukumbi wa mikusanyiko na mitihani, jengo la TEHAMA, nyumba za wafanyakazi, barabara za ndani nakadhalika. Miundombinu hii inahitaji fedha, ambazo zimekuwa adimu kupata.

Pili, Utafutaji wa fedha za kutosha kwa kwa ajili ya kufadhili wasichana wanaotoka kwenye familia zenye uhitaji umekuwa siyo rahisi. Hilo limeleta moja kwa moja athari katika kudahili na kusajili wanafunzi wahitaji hapa shuleni. Tayari JOHA TRUST imelazimika kukubali hali halisi na kupunguza idadi ya wasichana wanaofadhiliwa kutoka 100% mwaka 2000 tulipoanza hadi 10% mwaka huu 2019.

Changamoto kubwa zaidi ni kudumisha viwango vya ubora kwa bajeti finyu iliyopo.

Mheshimiwa Mgeni wetu Rasmi;
Katika majukumu uliyo nayo leo ni pamoja na kutunuku makundi mbalimbali. Tunao wafanyakazi waliodumu kazini kwa muda mrefu wa miaka 10 na 15. Pia tunaye mfanyakazi bora wa mwaka 2019. Hawa tutaomba uwape tuzo kama ishara ya shukrani kwa kufanya vizuri zaidi ya wengine na kutambua mchango wao kwa shule. Halikadhalika wapo wanafunzi ambao utawapa tuzo kwa kufanya vizuri kwenye masomo, uongozi, nidhamu, michezo, n.k. Hatimaye tutakuomba uwatunuku vyeti wahitimu wetu wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;
Kwa ridhaa yako naomba sasa niwageukie wanafunzi wahitimu. Wasichana hawa 87 wa kidato cha nne walioko mbele yenu wamepiga hatua moja katika maisha. Tumekuja hapa leo kuwapongeza , kutambua mafanikio waliyofikia, kusheherekea safari yao hii ya kimasomo, lakini pia kuwakumbusha tunawaamini. Kwa mtazamo wetu, lengo la elimu, siyo tu kuwasaidia wanafunzi kuelewa vema ulimwengu huu lakini kuwafanya wanaoelimishwa kupata shauku ya kufanya ulimwengu huu kuwa mahali pazuri pa kuishi kupitia ujuzi na maarifa waliyo nayo. Hivyo wakati tunatathmini na kuangalia nyuma kwenye yote yaliyotufikisha hapa leo, tunaangalia pia mbele yetu tukiwa na matumaini makubwa kuwa wasichana wetu tumewaandaa vema kwa hatua nyingine ya safari yao hii ya kielimu.

Enyi wanangu mnaohitimu*;*
Mimi naamini baada ya miaka minne ya kuwa nasi kwa elimu ya sekondari, mmekuwa tunu bora, adimu na za kipekee.

Mkiwa hapa shuleni sisi walimu wenu tuliwafanya mtumie akili zenu kufikiri kwa umakini na ubunifu, kutatua changamoto kupitia uvumbuzi, kushiriki katika kubadilishana mawazo ambako kulifungua njia mpya za kufikiri na mitazamo. Hivyo wakati mnapoanza kuchukua hatua nyingine ya kielimu maishani msiruhusu hofu kuwarudisha nyuma.

Ni lazima muendelee kutafuta… kujifunza ni kutafuta, kutafuta elimu, kutafuta kuelewa, kuuliza maswali na kutafuta majibu, kuvumbua vitu vinavyokuzunguuka ambavyo vitachochea fikra.

Kumbukeni kuwa wazazi wenu waliwapaka rangi za upinde wa mvua kupitia upendo na kujitoa kwao. Nanyi onesheni shukrani na upendo kwa wazazi wenu kwa kufanya vizuri katika masomo yenu na hatimaye mkaifanye dunia hii kuwa mahali pazuri pa kuishi.

Wapendwa wanafunzi;
Tunajua kuwa hakuna wawili kati yenu wanaolandana kwa kila kitu. Kila mmoja wenu ana fikra na ndoto zake ambazo zitahamisisha wengine maishani. Fikra zenu zitawapa nguvu wengine nao kufikiri, Vipawa na vipaji vyenu vitawafanya wengine nao kuwa wabunifu, uimara wenu utawafanya wengine kuiga uvumilivu. Najua ya kwamba ninyi kama binadamu, kila mmoja wenu anao uwezo na nguvu za kipekee sizofanana na mwingine. Kila mmoja wenu ajue kwa uhakika kuwa sauti yake ni muhimu kama ya mwingine ye yote yule na tuna imani kuwa mna mengi ya kuchangia katika dunia hii.

Tafadhali kumbatieni mabadiliko na tumieni fursa zitakazojitokeza mbele yenu. Kuweni na uthubutu wa kufanya mambo magumu na hayo yatawasaidia kukua katika uzoefu. Mkumbuke ya kwamba maisha ni tunu adimu kwa hiyo ni vema kutambua uzuri wa ulimwengu huu unaotuzunguuka. Wapende watu bila kificho, lia ikibidi bila woga wa kuhukumiwa na ye yote na achia sauti ya kicheko chako ijaze chumba. Usisite kuhurumia na kusaidia wengine kwani jambo hili litakuweka huru na kubaini tofauti kati yako na wale wasio na huruma na kukufanye utambue utu wa kila mtu.

Leo inaweza kuonekana kama vile mmefika kwenye ufukwe wa bahari. Mawimbi yetu hapa Barbro yamewatengeneza na kuwalea na sasa yatawabeba mbele katika safari yenu ya kielimu.

Wahitimu wetu,
Tunawapenda wote na tunajivunia sana ninyi. Enendeni mkawe mashujaa wetu sasa na siku zote. Asanteni sana kwa kuwa darasa jema, nawapongeza sana kwa siku ya leo na kuwatakia kila la kheri katika mitihani yenu ya taifa na safari yenu ya kimasomo.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mabibi na Mabwana;
Napenda kuhitimisha kwa kusisitiza kuwa tunahitaji nguvu za pamoja kwa maendeleo endelevu ya Shule ya Barbro na taifa kwa ujumla. Karibuni tuifurahie pamoja siku hii ya muhimu na ya kihistoria.

Asanteni kwa kwa kunisikiliza.